



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**MWALIKO KWA WATAZAMAJI WA NDANI WA UCHAGUZI
MDOGO KATIKA KATA SITA ZA TANZANIA BARA (LYOWA,
KILEO, VUMILIA, NERUMA, LUDUGA NA KAGERA-NKANDA)**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Madiwani tarehe 09 Oktoba, 2021 katika Kata zifuatazo. Kata ya Lyowa - Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Kileo - Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Vumilia - Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Neruma - Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Luduga - Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, na Kagera-Nkanda - Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Kwa kuzingatia kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kualika na kusajili watazamaji wa uchaguzi wanaotaka kutazama uchaguzi.

Kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kualika taasisi na asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama uchaguzi mdogo katika kata tajwa hapo juu.

Asasi na taasisi zenye nia ya kutazama uchaguzi huo zinatakiwa kuwasilisha maombi kwa kutumia Mfumo wa Menejimenti ya Watazamaji (OMS) kupitia "link" ifuatayo: <https://oms.nec.go.tz>

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha yafuatayo:-

- (i) Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;

- (ii) Mahali au sehemu ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (Physical address);
- (iii) Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
- (iv) Kata ambazo asasi au taasisi inataka kufanya zoezi hilo la utazamaji.
- (v) Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao;
- (vi) Majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili wa taasisi au asisi;
- (vii) Ikiwa taasisi au asasi inahusisha watendaji wa kimataifa wawili lazima wawe watanzania;
- (viii) Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
- (ix) Kuambatisha nakala au kivuli cha Katiba ya taasisi au asasi husika.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09 Septemba, 2021

Imetolewa leo tarehe 03/09/2021 na;



Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

Tarehe 03/09/2021